

Kwa nini mwanamke katika uislamu anarithi nusu ya kile anachorithi mwanaume?

Mwanamke kabla ya uislamu alinyimwa mirathi, wakati uislamu ulipokuja ukamjumuisha katika mirathi bali yeye anaweza kupata fungu kubwa kuliko wanaume au wakagawana sawa kwa sawa. Mwanamke baadhi ya wakati atarithi na mwanaume asirithi Wanaume hupata fungu kubwa kuliko wanawake kulingana na ukaribu walionao na marehemu na fungu katika hali nyingine , ndio hali inayoelezwa katika Quran tukufu:

Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili..."[210]. (AN-NISAAI 11)

Bibi mmoja muislamu siku moja alisema hakuwa akielewa jambo mpaka alipofariki baba mkwe wake, mumewe alirithishwa mara mbili ya kile alichorithi dada yake(wifi yake), mumewe akanunu kuitia urithi huo vitu ambavyo hakuwa navyo kama vile nyumba ya familia yake na gari. Dada naye akanunua johari/vito pesa nyingine akaziweka benki, huku mumewe ndio mwenye jukumu kuhakikisha wanapata makazi na mahitaji mengine ya muhimu. Sasa hivi akafahamu hekima ilipo nyumba ya hii hukumu. Akasema Alhamdulillah.

Hata kama katika jamii nyingi mwanamke anafanya kazi kwa ajili ya kuendesha familia hukumu ya wanamke katika hili haiondoki. Mfano simu imeharibika kwa sababu mtumiaji ameshindwa kufuata masharti ya matumizi ya simu ,sio hoja ya kuwa hayo masharti kutofaa.

سؤال وجواب حول الإسلام

Source: <https://www.mawthuq.net/demo/qa/sw/show/89/>

Arabic Source: <https://www.mawthuq.net/demo/qa/ar/show/89/>

Friday 4th of July 2025 09:24:00 AM